# SURA YA TANO

# NILITULIA NA KURIDHIKA

"*Usiridhike na chochote chini ya kile unachotaka*" PJ Harvey

Vitu ambavyo hatukuvifanya vinaweza kuwa ndiyo sababu kuu ya kuto kufanikiwa katika maisha yetu kuliko hata tulivyofanya. Watu wengi wameridhika na maisha wanayoishi sasa. Hata mimi nilikuwa katika bwawa hilo hilo la watu walioridhika na maisha. Nimekuwa nikifanya uchunguzi watu wanasema nini kuhusu maisha yao. Nilipowahoji mnasema nini kuhusu maisha? Nilipata majibu haya, "aha bwana sina cha kufanya maisha yamegoma". Wengine walisema "maisha magumu sana kila ukijitahidi lakini wapi." Wengine walisema, "mzee hapa duniani hatuwezi kuwa matajiri wote nani atamfanyia mwenzake kazi". Jillian Michaels alisema, "***uwe wa kushangaza, Ishi kikamilifu, Lenga nyota na kamwe usitulie."***

Nimekwambia mimi nililidhika kama watu wengine walivyoridhika. Sikuwa tayari kujiuliza maswali magumu na ya msingi. Mfano wa maswali hayo ni haya yafuatayo, "**je *maisha yangu ndiyo haya ama nina uwezo wa kuyabadilisha? Je kuna mtu ninaye msubiri aje abadilishe maisha yangu? Je ningependa maisha yangu yaweje baadaye? Je naweza kuanzia wapi kubadilisha maisha yangu***.

Nakuomba na wewe leo hii ujiulize maswali hayo. Watu wengi wameridhikka sana na maisha yao. Watu hawa ndiyo nilioishi nao. Na kwa kuwa mtu huwa kama watu anaoshi nao muda wote basi waliniathiri sana kifikra. Niliridhika na kuyaona maisha yangu ni bora na ndani yangu halikuwaka hitaji la kutaka kuishi maisha mengine zaidi ya haya. Sikuwa tayari kujiuliza nifanye nini ili kuanza kuboresha maisha yangu? Lakini pia sikuwa tayari kujifunza ujuzi mpya na hata kujifunza namna ya kutunza na kutumia fedha. Kitu ambacho nimejifunza ni kwamba watu wa kawaida wanataka kubaki salama na kutulia bila kufikiria kufanya kitu kingine zaidi ya kile walichozoea.Tony Gaskins alisema, ***"Jijue wewe ni nani. Jua unachohitaji. Jua unachostahili. Na usiridhike na kilicho pungufu."*** Lakini matajiri wao wako tayari kutoka katika ukanda wa kutulia na kutaka kufanya kazi mpya ili kubadili maisha yao. Wako tayari kujaribu fursa mpya na kuiwekea mipango kabambe ya kuifanikisha. Matajiri wanajua kuwa hata kama maisha yako hivi leo lakini yanaweza kubadilishwa na mhusika. Wako tayari kufanya kitu kipya na wakikutana na kushindwa hawakati tama, wanajua hiyo ni nafasi ya kujifunza. Matajiri wanajua kwamba, kuufikia utajiri siyo rahisi na hakuna kutulia katika safari ya kuusaka.

Wanajua kwamba ni vema kutulia katika safari ya kutokutulia. Wako tayari kuingia msituni na kukutana na mambo yasiyotarajiwa. Tabia hizi za matajiri ndiyo tabia ambazo ilinibidi niziige katika maisha ya sasa. Wao hawaogopi chochote. Mark Cuban alisema, ***Usitulie hakuna haja ya kuharakisha."*** Siku hizi baada ya kubadilika nikipanga kufanya kitu sikai na kujiuliza tena maswali nifanye au nisifanye.

Nimejifunza kuwa kila kitu kinawezekana. Nimejifunza kwa matajiri wao wanaamini kuwa mipango ambayo maskini wanaona kuwa ni migumu, matajiri huamini kuwa wanaweza kuifanya ikaleta matokeo. Hakuna mtu aliyetegemea kuwa mimi ninaweza kuwa ni mhamasishaji, wala kuwa mwandishi. Bali nilisema lazima nibadilishe maisha yangu, lazima nifanye kitu kipya ambacho nilikuwa sikifanyi. Niliamua kujitoa kikamilifu mzimamzima. Niliamua kujifunza sanaa hii ya kuhamasisha na pia kuwa mwandishi.Nilijiamini, nilijipa hadhi mpya, na nilidhamilia kuwa tofauti kwa gharama yoyote. Kumbuka kuwa mimi leo nina miaka sitini na mbili. Sijiangalii nina miaka mingi ila nataka kuona nafanya kitu cha maana kwa ajili ya jamii.

Nilipokuwa kijana nilitakiwa niwe na maono makubwa na hivyo nisingeweza kutulia. Malengo makubwa yanamfanya mtu atoke nje ya ukanda wa kutulia. Kama ningejenga mienendo na tabia za matajiri ni wazi ningekuwa mbali na kuwa milionea. Ndugu unayesoma kitabu hiki usilidhike na maisha uliyonayo. Anza kujifunza ujuzi mpya na anza kupata maarifa mapya ambayo yatakusaidia kuyapandisha maisha kutoka kiwango chako cha sasa na kuyapeleka kiwango cha juu zaidi. **Hata wewe usikubali kuendelea kutulia bila kuchukua hatua yoyote ya kubadilisha maisha yako. Acha kulidhika na kutulia wakati maisha yako bado hayaridhishi.**